# PDPC FARAGHA NEWSLETTER

Toleo Na. 0001 Aprili - Juni 2025




Dkt. Emmanuel Mkilia
**Mkurugenzi Mkuu - PDPC**

## TAASISI KUJISAJILI PDPC NI TAKWA LA KISHERIA

UK. 06

RIDHAA INAPASWA KUTOLEWA BILA SHURUTI. UK. 7

## Makala Maalumu - PDPA

UK.17

SIMAMIENI MIPANGO YA KUPUNGUZA VIHATARISHI KWENYE ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

PDPC YATOA MAFUNZO KWA WANAFUNZI WA VYUO VYA TEHAMA

WATUMISHI WA PDPC WAPATIWA MAFUNZO KUHUSU PDPA

# YALIYOMO

UK. 06 Taasisi kujisajili PDPC ni takwa la kisheria

UK. 07 Simamieni mipango ya kupunguza vihatarishi kwenye Ulinzi wa Taarifa Binafsi

UK. 08 DPIA ni lazima, kabla ya kuanzisha mradi unaokusanya na kuchakata Taarifa Binafsi nchini

UK. 14 Watumishi wa PDPC wapatiwa mafunzo kuhusu PDPA

UK. 15 PDPC yavitaka vyama vya siasa kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi za wanachama wao





## SALAMU KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU WA TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

**Ndugu Msomaji,**

Ni furaha kubwa kwangu kukusalimu kupitia toleo hili la kwanza la jarida la "Ulinzi wa Taarifa Binafsi". Jarida hili ni sehemu muhimu ya mkakati wa Tume kuhakikisha kuwa jamii inapata elimu sahihi kuhusu masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi, haki ya faragha, na wajibu wa wadau katika kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya 2022.

Katika dunia ya sasa yenye maendeleo makubwa ya kidijitali, elimu kwa umma kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha usalama wa taarifa za watu. Wananchi wanapaswa kufahamu jinsi ya kulinda taarifa zao, madhara yanayoweza kujitokeza endapo zitadhibitiwa vibaya, na hatua zinazopaswa kuchukuliwa pale ambapo haki yao ya faragha inavunjwa. Jarida hili litakuwa chombo cha kuhamasisha, kuelimisha na kuhimiza uwajibikaji katika usimamizi wa taarifa binafsi.

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa ulinzi wa taarifa binafsi unazingatiwa katika sekta zote. Kupitia jarida hili, tutakuwa tukitoa taarifa kuhusu matukio mbalimbali, mafanikio ya utekelezaji wa sheria, na changamoto zinazojitokeza ili kujenga jamii yenye uelewa mpana wa haki na wajibu wao katika kulinda taarifa binafsi.

Natoa rai kwa kila mmoja kushiriki kikamilifu katika safari hii ya kulinda taarifa binafsi kwa manufaa ya taifa letu. Tunakaribisha maoni, ushauri, na michango yenu katika kuboresha jarida hili na kuhakikisha linakuwa na mchango chanya kwa jamii.

Asanteni kwa kuunga mkono juhudi za ulinzi wa taarifa binafsi nchini.

**Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia**
Mkurugenzi Mkuu



# BODI YA WAHARIRI



**Mwenyekiti**
**Dkt. Emmanuel Mkilia**



**Mjumbe**
**Mhandisi Stephen Wangwe**



**Mjumbe**
**Wakili Humphrey Mtuy**



**Mjumbe**
**Dkt. Noe Nnko**



**Mjumbe**
**Rehema Abdallah**



**Mhariri Mkuu**
**Innocent Mungy**

# TAHARIRI YA MHARIRI



Karibu kwenye toleo la kwanza la jarida la "Ulinzi wa Taarifa Binafsi", jarida rasmi la Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC). Jarida hili limeanzishwa kwa dhamira ya kuwa chanzo cha taarifa sahihi, elimu, na mwongozo kwa umma kuhusu dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi, wajibu wa wadau mbalimbali, na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA) pamoja na Kanuni zake.

Katika dunia ya sasa, ambapo matumizi ya teknolojia ya kidijitali yanaongezeka kwa kasi, suala la ulinzi wa taarifa binafsi limekuwa muhimu kuliko wakati wowote ule. Taarifa binafsi zina thamani kubwa na zinapaswa kulindwa kwa mujibu wa sheria ili kuzuia matumizi mabaya, ukiukwaji wa faragha, na madhara yanayoweza kusababishwa na upatikanaji usio halali wa taarifa hizo. Ndiyo maana Tume imejizatiti kuhakikisha kuwa sheria inatekelezwa kwa ufanisi, huku tukitoa elimu kwa umma na wadau mbalimbali ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu haki na wajibu wao.

Jarida hili litatolewa kila robo mwaka likihusisha habari, tafiti, na matukio muhimu yanayohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi ndani ya kipindi husika. Katika toleo hili la kwanza, tutakuletea muhtasari wa hatua zilizochukuliwa tangu kuanzishwa kwa Tume, mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizojitokeza, na mwelekeo wa siku zijazo. Vilevile, tutakuwa na makala maalum zinazofafanua dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi, hadithi za mafanikio, na maoni kutoka kwa wataalamu wa sekta mbalimbali kuhusu umuhimu wa kulinda taarifa za watu.

Tume inaamini kuwa kila mtu ana wajibu wa kushiriki katika kulinda taarifa binafsi, iwe ni taasisi za umma, sekta binafsi, au wananchi kwa ujumla. Hivyo basi, tunakukaribisha usome na kushiriki mawazo yako nasi ili kwa pamoja tujenge jamii inayotambua thamani ya faragha na haki ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Tunaahidi kuendelea kuwaletea maudhui yenye tija, maarifa, na mwongozo wa kitaalamu ili kuhakikisha kuwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inatekelezwa ipasavyo kwa manufaa ya wote. Endelea kufuatilia jarida hili kwa habari na uchambuzi wa kina kuhusu maendeleo ya ulinzi wa taarifa binafsi nchini Tanzania.

**Innocent P. M. Mungy**
**Mhariri Mkuu**
**Jarida la "Ulinzi wa Taarifa Binafsi"**

## TUMIENI TEKNOLOJIA VIZURI KULINDA TAARIFA BINAFSI

Taasisi nchini zimetakiwa kuzingatia matumizi ya teknolojia zinazowezesha kulinda taarifa ili kuhakikisha hakuna uvunjifu wa Sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi nchini.

Hayo yalisemwa kwenye warsha ya ulinzi wa taarifa iliyofanyika jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujadili teknolojia zinazoweza kusaidia kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi kwenye taasisi nchini Tanzania wakati taasisi hizo zikianza kutekeleza sheria hiyo ya ulinzi wa taarifa binafsi ya mwaka 2022.

Akizungumza kwenye warsha hiyo, Mkurugenzi wa Kitengo cha Tafiti za Ulinzi wa Taarifa na Teknolojia kutoka Tume ya Ulinzi wa taarifa binafsi (PDPC), Dkt. Noe Nnko amezitaka taasisi za umma na binafsi nchini kuhakikisha zinazingatia sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa kutumia teknolojia vizuri na kulinda taarifa hizo.

"Taasisi zote za umma na binafsi lazima zihakikishe zimejisajili na kupata cheti cha PDPC kabla ya Disemba, 2024 ili kutii maagizo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuheshimu sheria kwani kutokufanya hivyo ni kosa" Alisema Dkt. Nnko



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), **Dkt. Emmanuel Mkilia** (Alievaa Miwani) akifatilia Mjadala wa Umuhimu wa Matumizi ya Akili Unde kwa Wanahabari. Mjadala huo ulifanyika kwenye Maadhimisho ya siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, yaliofanyika kitaifa April 29, 2025 , Jijini Arusha ambapo Mgeni Rasmi alikua Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa.

## TAASISI KUJISAJILI PDPC NI TAKWA LA KISHERIA

**W**akati dunia ikisherehekea maadhimisho ya siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imetahadharisha kuwa taasisi zote za umma na binafsi nchini zinapaswa kuwa zimesajiliwa rasmi kabla ya tarehe 30 Aprili 2025. Hii ni baada ya ukomo wa awali wa usajili ulioelezwa kuisha tarehe 31 Desemba 2024, ambapo zoezi la usajili liliongezwa muda kwa hiari.

Katika mjadala huo uliohudhuriwa na Taasisi za Serikali zinazoshughulikia masuala ya habari, teknolojia, na ulinzi wa faragha, Dkt. Mkilia amesisitiza kwamba sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi haikusudii kuzuia au kukwamisha sheria nyingine kama ile ya Haki ya Kupata Habari au Uhuru wa Vyombo vya Habari na Uhuru wa Kujieleza bali kuhakikisha faragha na taarifa binafsi zinalindwa.

“Sheria hii inalenga kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari na haki ya wananchi kupata habari, huku ikihakikisha faragha ya watu inahifadhiwa. Wajibu wetu ni kuhakikisha kuwa taarifa binafsi za watu zinazingatiwa na zinalindwa kikamilifu,” alisisitiza Dkt. Mkilia.

Akiendelea kuzungumza katika maadhimisho hayo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Dkt. Emmanuel Mkilia, amesema dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi pia ni muhimu kwa waandishi wa habari na wadau wa sekta hiyo, ikiwa ni sehemu ya kufuata sheria na kanuni za uandishi wa habari pamoja na sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi.

“Uandishi wa habari ni taaluma inayofuata misingi ya haki na ukweli, hivyo ni wajibu wa kila mwandishi kuzingatia matakwa ya sheria hizi ili kuhakikisha uhuru wa vyombo vya habari na haki ya wananchi kupata habari unafikiwa,” alisema Dkt. Mkilia.

Maadhimisho ya mwaka huu yana kauli mbiu inayosisitiza mustakabali wa uhuru wa vyombo vya habari unaoambatana na uwajibikaji, huku ikilenga kuhimiza usalama wa haki za wanahabari na wananchi kwa ujumla, wakati huu wa ukuaji wa kasi wa Teknolojia na matumizi ya Akili Unde, ikisisitiza matumizi ya teknolojia na ubunifu katika kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka 2025 ni: “Uandishi wa Kijasiri na Mustakabali wa Uhuru wa Vyombo vya Habari wakati huu wa matumizi ya Akili Unde ” Kauli mbiu hii inalenga kuhimiza uelewa na umuhimu wa teknolojia na ubunifu katika kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari, huku ikilenga pia kuimarisha uwajibikaji na ufanisi wa sekta hiyo.

> **“Wajibu wetu ni kuhakikisha kuwa taarifa binafsi za watu zinazingatiwa na zinalindwa kikamilifu.**
>
> Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu - PDPC

# SIMAMIENI MIPANGO YA KUPUNGUZA VIHATARISHI KWENYE ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia amezitaka taasisi za umma na binafsi nchini kusimamia mipango ya kupunguza vihatarishi katika ulinzi wa taarifa binafsi.

Dkt. Mkilia ameyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya kupunguza vihatarishi katika ulinzi wa taarifa binafsi kwa wasimamizi wa vihatarishi wa taasisi za umma na binafsi yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Lush Garden iliyopo jijini Arusha.

“Kusudio la mafunzo haya si kuongeza maarifa tu kwenye kazi, bali ni hatua ya kujenga utamaduni mpya wa usalama wa taarifa binafsi zinazokusanywa na kuchakatwa na Taasisi zenu” amesema Dkt. Mkilia

“Natoa wito kwenu kasimamieni na kuanzisha mipango ya ndani ya kupunguza vihatarishi katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi, fanyeni tathmini na kuboresha sera na mifumo yenu ya TEHAMA na shirikianeni na Tume kwa ukaribu katika kutoa taarifa na kupata ushauri wa kitaalamu kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi” amesema Dkt. Mkilia

Wakati huo huo, Katibu Mtendaji wa Chuo cha Usimamizi wa Vihatarishi (IRMT) Bw. Christopher Njovu ametoa rai kwa taasisi za umma na binafsi kuzingatia kupata elimu hiyo na kuhakikisha maafisa wao wanakuwa wataalamu walioidhinishwa kusimamia vihatarishi.

“IRMT tunatoa mafunzo ya kutengeneza na kuthibitisha wataalamu wa usimamizi wa vihatarishi nchini Tanzania, hivyo nawasihi mje mpate mafunzo haya na vyeti vya kuwathibitisha kuwa ni wataalam wa eneo hili” amesema Bw. Njovu

Mafunzo hayo ya siku tatu yaliyofanyika kuanzia tarehe 23 hadi 25 Juni, 2025 ni moja ya njia ya kuhakikisha taasisi za umma na binafsi zinakuwa na utaratibu wa kutambua viashiria vya vihatarishi hivyo na kuchukua hatua stahiki kabla hatari haijatokea.



Baadhi ya Viongozi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Chuo cha Usimamizi wa Vihatarishi (IRMT), **{Waliokaa}** wakiwa kwenye Picha ya pamoja na baadhi ya Washiriki wa Mafunzo ya kupunguza vihatarishi katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa wasimamizi wa vihatarishi kutoka Taasisi za Umma na Binafsi. Mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Lush Garden iliyopo jijini Arusha na yalifunguliwa rasmi na **Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Emmanuel Mkilia**




# RIDHAA INAPASWA KUTOLEWA BILA SHURUTI

Wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Nchini wameshauriwa kukusanya na kuchakata Taarifa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 (PDPA) ikiwa ni pamoja na kutowashurutisha wahusika wa Taarifa hizo kuwapatia ridhaa.

Wito huo umetolewa jijini Arusha Juni 24, 2025 na Wakili Humphrey Mtuy, Mkuu wa Kitengo cha Sheria,Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC). Wito huo ameutoa wakati akiwasilisha mada ya masuala muhimu ya kisheria katika PDPA kwa washiriki wa mafunzo ya kupunguza madhara ya vihatarishi katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambapo amesema kwa mujibu wa PDPA hairuhisiwi kuchukua ridhaa ya muhusika wa taarifa kwa shuruti.

“Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kifungu cha thelathini (30) kifungu kidogo cha Kwanza (1) na Kanuni ya Ishirini na Tano 25 (d) ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa imeanisha mazingira ya kuchukua ridhaa kwa muhusika wa taarifa hivyo inapaswa kutoa ridhaa bila shuruti,” amesema Wakili Mtuy



Aidha wakili Mtuy amesisitiza kuwa PDPA imekuja kumlinda muhusika wa Taarifa na imeruhusu PDPC kushirikiana na vyombo vingine vya dola kumpatia haki ya faragha muhusika wa taarifa endapo taarifa zake zitatumika vibaya.






## DPIA NI LAZIMA, KABLA YA KUANZISHA MRADI UNAOKUSANYA NA KUCHAKATA TAARIFA BINAFSI NCHINI

Mkurugenzi wa Tafiti za Ulinzi wa Taarifa na Teknolojia, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Noe Nnko amezitaka Taasisi zote nchini kuhakikisha wanafanya Tathmini ya Athari za Ulinzi wa Taarifa (DPIA) kabla ya kuanzisha mradi wowote unaokusanya na kuchakata Taarifa Binafsi nchini.

Dkt. Noe amesema hayo Juni 23, 2025 jijini Arusha wakati akiwasilisha mada ya kupunguza madhara ya vihatarishi katika ulinzi wa taarifa binafsi kwenye teknolojia zinazoibukia kwa washiriki wa mafunzo ya kupunguza madhara ya vihatarishi katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambapo amesema kufanya hivyo ni kutimiza moja ya takwa la Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 ambayo imeipa Mamlaka PDPC kupitia DPIA za miradi yote inayohusisha ukusanyaji na uchakataji wa Taarifa Binafsi.

“Tunapaswa kufanya Tathmini ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPIA) kabla ya kuanzisha Mradi wowote nchini kwa mfano wale wanaofungua viwanda hawawezi kufungua bila kushauriana au kuhakikiwa na NEMC vivyo hivyo huwezi kuanzisha Programu wezeshi yoyote (Application) bila kushauriana na PDPC kwakua Pragramu hiyo ikiwa na madhara kwenye Ulinzi wa Taarifa Binafsi haitaruhusiwa” amesema Dkt. Noe.

## STANBIC Benki, watembelea Ofisi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)




Mkurugenzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Ofisi ya Zanzibar, **Bi. Rehema Abdalla,** (Kushoto) akiwa na Baadhi ya Watumishi wa Benki ya Stanbic Tawi la Zanzibar, wakati walipotembelea Ofisi ya PDPC ili kupata Elimu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

Mkurugenzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Ofisi ya Zanzibar, Bi. Rehema Abdalla, amekutana na Viongozi wa Stanbic Benki - Zanzibar na kufanya nao mazungumzo kwa lengo la kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini.

Katika Mazungumzo hayo Bi. Rehema ameweka bayana majukumu ya PDPC ikiwa ni pamoja na kusajili, kuratibu na kusimamia wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi nchini ili kuhakikisha taarifa hizo zinakusanywa, zinachakatwa na kutunzwa kwenye mazingira salama.

Aidha Bi Rehema ametoa wito kwa mashirika na taasisi zote zinazotoa huduma visiwani Zanzibar kujisajili kwenye mfumo wa PDPC, ili kutimiza matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 (PDPA) ambayo inazitaka Taasisi na Mashirika yote yanayokusanya na kuchakata Taarifa nchini kusajiliwa na PDPC.

Kwa upande wake, Mkuu wa msafara kutoka Stanbic Benki Tawi la Zanzibar, Bi Fatma Ahmed, amesema Benki hiyo imedhamiria kulinda Taarifa Binafsi za wateja wake na wanaamini itasaidia kuimarisha biashara na kuleta huduma bora kwa wananchi wa Zanzibar.

# SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI INAZUIA MATUMIZI HOLELA YA TAARIFA ZA WANANCHI

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi sura ya 44 inalenga kulinda faragha za wananchi kwa kuzuia matumizi holela ya taarifa za wananchi ambapo kupitia Sheria hii muhusika wa Taarifa anapaswa kutoa ridhaa ya matumizi ya taarifa zake.

Hayo yamebainishwa jijini Dodoma, Aprili 29, 2025 na Mkurugenzi wa Usajili na Uzingatiaji, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Mhandisi Stephen Wangwe, wakati akizungumza kwenye kikao cha kupokea maoni kuhusu rasimu ya Kanuni za Ada za Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2025 ambapo amesema Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inalenga kulinda faragha za wananchi kwa kuzuia matumizi holela ya Taarifa zao na akatolea mfano wa watu kupigwa picha au video katika hafla kama harusi au misiba bila ridhaa yao na picha hizo kusambazwa mitandaoni.

Naye Mkurugenzi wa PDPC - Ofisi ya Zanzibar, Bi. Rehema Abdallah, amesema uwepo wa Sheria hiyo utaziwezesha Taasisi za Zanzibar kushiriki kikamilifu katika kulinda faragha za wananchi pamoja na kupanua wigo wa usimamizi wa Taarifa Binafsi na itaongeza imani kwa watumiaji wa huduma za kidijitali kutokana na uhakika wa Ulinzi wa Taarifa na faragha zao.

Akizungumza wakati wa kufungua kikao hicho, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi





wa Rasilimali watu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Bi. Salome Kessy, amesema kuwa kanuni hizo zitasaidia kuimarisha Ulinzi wa faragha za wananchi ambayo ni haki yao ya kikatiba na akaweka bayana kuwa utekelezaji wa sheria hii unakwenda sambamba na maono ya 4R za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.




**HABARI PICHA:**
Mkurugenzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Ofisi ya Zanzibar, Bi. Rehema Abdalla akiwakabidhi Vyeti vya Ushiriki baadhi ya washiriki wa mafunzo ya kupunguza madhara ya vihatarishi katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Mafunzo haya yaliandaliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa kushirikiana na (IRMT) Taasisi ya Usimamizi wa Vihatarishi Tanzania kwa lengo la kuongeza uelewa na ujuzi wa namna bora ya kulinda Taarifa Binafsi kwa kuzingatia usimamizi wa vihatarishi na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44, Kanuni zake pamoja na Miongozo ya PDPC.






























**HABARI PICHA:**
Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya kupunguza madhara ya vihatarishi katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi wakifatilia mada katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa kushirikiana na Taasisi ya Usimamizi wa Vihatarishi Tanzania (IRMT).

Mafunzo haya yalifanyika kuanzia tarehe 23, 2025 hadi 25 Juni, 2025 jijini Arusha..





















**HABARI PICHA:**
Rehema Abdalla, Mkurugenzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Ofisi ya Zanzibar (alievaa kitenge) pamoja na Timu ya Wataalamu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka Mradi wa Twinning wakiwapongeza baadhi ya watumishi wa PDPC baada ya kuhitimu mafunzo maalumu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA).

Felix Wagner, Anna-Lena Greve, Jani Ruuskanen na Mika Koponen ni miongoni mwa Wataalamu hao wa PDPA.



**HABARI PICHA:**
Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia (Kushoto) akiteta jambo na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, kabla ya kuanza kikao cha siku mbili cha Baraza la Vyama vya Siasa leo tarehe 14 Mei, 2025 mjini Morogoro, ambapo moja ya mada zilizowasilishwa kwenye siku ya kwanza ya kikao hicho ni umuhimu wa kutunza taarifa binafsi hususani katika kipindi hiki ambacho Tanzania inaelekea kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2025.





Baadhi ya Washiriki wa kikao cha siku mbili cha Baraza la Vyama vya Siasa wakifatilia Mada mbalimbali za Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka kwa Wakufunzi ambao ni watumishi wa PDPC.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia akizungumza na washiriki wa kikao cha Baraza la Vyama vya Siasa kilichofanyika Mjini - Mei 14, 2025



Dkt. Noe Nnko, Mkurugenzi wa Tafiti na Teknolojia za Taarifa - Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), akiwasilisha mada ya Changamoto za Teknolojia zinazoibukia katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwenye kikao cha Baraza la Vyama vya Siasa kilichofanyika Mkoani Morogoro - Mei 14, 2025.



Mhandisi Stephen Wangwe, Mkurugenzi wa Usajili na Uzingatiaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), akiwasilisha mada ya Muhtasari wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA) kwenye kikao cha Baraza la Vyama vya Siasa kilichofanyika Mkoani Morogoro - Mei 14, 2025.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia (Watatu kutoka kushoto) akiwa na Baadhi ya washiriki wa kikao cha wadau cha kujadili na kutoa maoni kuhusu Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Mtandao pamoja na Mkakati wa Taifa wa Ulinzi wa Mtoto Mtandaoni, kilichofanyika jijini Dodoma Mei 08, 2025.






Baadhi ya watumishi wa Tume ya ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) wakiwa kwenye maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani (MEI MOSI) yaliyofanyika kitaifa Mkoani Singida, tarehe 01/05/2025.

## WATUMISHI WA PDPC WAPATIWA MAFUNZO KUHUSU PDPA

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imeendelea na jitihada zake za kuhakikisha elimu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inawafikia wananchi wote nchini.

Juni 17, 2025 jijini Dodoma PDPC kwa kushirikiana na Digitali kwa Tanzania (D4T) kupitia mradi wa Twinning wametoa mafunzo maalum kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPA) kwa watumishi wa Tume hiyo kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na umuhimu wa Kulinda Taarifa Binafsi kwenye wakati huu wa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia Duniani.

Mafunzo hayo ya siku nne (4) yalifunguliwa na Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa PDPC ambapo amesema kupitia mafunzo haya watumishi wa PDPC watapatata nafasi ya kuifahamu vema Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo wanaitumia kuhakikisha faragha za watu zinalindwa.

Kwa Upande wake Bw. Jani Ruuskanen, Mshauri Mkaazi wa Digitali kwa Tanzania (D4T) katika Mradi wa Twinning amewataka watumishi hao wa PDPC kutumia mafunzo haya kujifunza mengi kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwakua wakufunzi wake ni wataalamu wabobevu kwenye sekta hiyo hivyo wasisite kuuliza maswali mengi kadiri wawezavyo ili kujifunza.

Mafunzo hayo ni sehemu ya kuhakikisha PDPC inaendelea kuwa na matokeo chanya katika Sekta ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini.



Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) akizungumza na Watumishi wa PDPC wakati wa Mafunzo Maalumu ya PDPA yaliyofanyika Jijini Dodoma, Juni 17 - 20, 2025.



Baadhi ya watumishi wa PDPC na Wakufunzi kutoka D4T wakiwa kwenye picha ya pamoja

## PDPC YATOA MAFUNZO KWA WANAFUNZI WA VYUO VYA TEHAMA

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imefanya semina kwa wanafunzi wa vyuo Vikuu vinavyofundisha masomo ya TEHAMA vilivyopo kwenye Mkoa wa Dar es Salaam ikiwa ni jitihada za kutoa elimu ili kujenga uelewa kuhusu dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi nchini.

Mafunzo haya yamefanyika katika ukumbi wa Maktaba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ambapo watumishi wa Tume, akiwemo Mkurugenzi wa Usajili na Uzingatiaji, Mhandisi Stephen Wangwe, pamoja na Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano, Bw. Innocent Mungy, walifundisha mbinu mbalimbali za kulinda taarifa binafsi hususani katika kipindi hiki cha kukua kwa teknolojia zinazoibukia.

Lengo la mafunzo haya ni kuhakikisha wanafunzi wanajua jinsi ya kulinda Taarifa zao Binafsi ili zisije kutumiwa vibaya na kuingilia faragha zao kitendo kitakacholeta matokeo ya uvunjifu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44.



Bw. Innocent Mungy, Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) akitoa Elimu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa binafsi kwa baadhi ya wanafunzi wa vyuo Vikuu vinavyofundisha masomo ya TEHAMA vilivyopo jijini Dar es Salaam.

# PDPC YAVITAKA VYAMA VYA SIASA KUHAKIKISHA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI ZA WANACHAMA WAO



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia, ameelezea umuhimu wa vyama vya siasa kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi za wanachama na wafuasi wao. Ameyasema hayo katika Mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa ulilofanyika katika hoteli ya NASHERA, Morogoro.


Dkt. Mkilia alieleza kuwa, kwa mujibu wa Ibara ya 16(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila mtu faragha yake ina haki ya kuheshimiwa na kutunzwa katika maisha yake. Hii inaashiria kuwa taarifa zinazomhusu mtu huyo kama ni jina, namba za simu, anwani, itikadi za kisiasa, au hali ya kiafya zinapaswa kulindwa dhidi ya matumizi yasiyo halali au usambazaji holela.

Aidha, alitahadharisha kuhusu hatari zinazoweza kuvikumba vyama vya siasa kama havitazingatia misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi, ikiwa ni pamoja na kuchukua taarifa za wanachama bila ridhaa yao, kutangaza majina au picha bila kibali, na kuuza orodha za wanachama kwa maslahi ya kisiasa. Hii ni kinyume na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022, inayowataka taasisi zote zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi kuzingatia maadili na uwazi.

Ni muhimu vyama hivyo vijisajili PDPC, viwe na sera za faragha zinazoainisha taarifa gani zinakusanywa, kwa nini, na jinsi zitakavyohifadhiwa ili kuhakikisha taarifa za wanachama wao zinalindwa kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kuimarisha usalama wa taarifa nyeti, kujenga imani kwa wananchi na kuweka mazingira salama ya ushiriki wa kisiasa bila hofu ya kuvujisha au kutumia taarifa binafsi kwa njia isiyo halali.

Aidha, Msajili wa Vyama vya Siasa Mhe Jaji Francis Mutungi, amevitaka vyama vya siasa kuzingatia sheria za nchi pamoja na katiba zao za ndani katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwani kutofanya hivyo kuna pelekea migogoro isiyo ya lazima inayoweza kuzuilika kwa kufuata taratibu zilizowekwa kisheria.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Mhe Juma Khatibu amesema kuwa ulinzi wa taarifa binafsi ni moja ya vigezo vya msingi vinavyojenga jamii inayothamini utu wa kila mtu.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

PDPC

## TAARIFA KWA UMMA

**UVUNJWAJI WA FARAGHA NA UKIUKWAJI WA TAARIFA BINAFSI ULIOONEKANA KWENYE MACHAPISHO YA UMMA HUSUSANI MITANDAO YA KIJAMI**

**Dodoma, Tanzania – Mei 24, 2025**

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi **(PDPC)** inapenda kuuarifu umma kuwa, kufuatia ufuatiliaji wake wa kawaida chini ya mamlaka iliyoainishwa katika kifungu cha 7(a) cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA), hivi karibuni imebaini ukiukwaji wa masharti ya Sheria husika hali iliyopelekea uvunjifu wa faragha na uvujishaji wa taarifa binafsi katika machapisho mbalimbali ya umma.

Taarifa hii inalenga kuujulisha umma kuwa, Tume, kwa mujibu wa kifungu cha 7(d) cha PDPA, imeanzisha uchunguzi rasmi wa tukio hilo ili kubaini chanzo, aina na ukubwa wa ukiukwaji huo ambao ni kinyume cha sheria na unaweza kusababisha hatua za kisheria ikiwemo, faini au adhabu za kiutawala, mashauri ya kisheria na maagizo ya marekebisho ya lazima. Kutokuzingatia sheria hakutavumiliwa na watakaobainika watawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Tume inachukulia suala hili kwa uzito mkubwa na imejizatiti kuhakikisha kuwa taarifa binafsi zinakusanywa na kuchakatwa kwa mujibu wa sheria, kwa usalama na kwa kuheshimu haki za mtu binafsi.

Kwa mantiki hiyo, Tume inazikumbusha taasisi zote za umma na binafsi kuwa:

1. **Zinapaswa kufuata kikamilifu masharti ya Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi** na kanuni zake.
2. **Kuhakikisha kuwa sera zao za ndani za faragha zimesasishwa** na zinaendana kikamilifu na sheria.
3. **Kufanya mafunzo ya uelewa kwa wafanyakazi wao mara kwa mara** ili kuhakikisha wanaelewa vyema wajibu wao katika kulinda taarifa binafsi.

Kulinda taarifa binafsi si tu ni jukumu la kisheria, bali ni msingi muhimu wa kujenga imani kwa huduma za serikali na sekta binafsi. Taasisi zitakazoshindwa kuweka na kutekeleza hatua stahiki za kulinda taarifa binafsi zitawajibishwa kwa mujibu wa Sheria.

Tume inatoa wito kwa wadau wote kutoa ushirikiano wakati uchunguzi ukiendelea.

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu**

**Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)**

**"FARAGHA YAKO NI WAJIBU WETU"**

Jengo la UCSAF , Barabara Namba. 10, S. L.P 1105, Dodoma - Tanzania

Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.

@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz



# HATUA ZA KUSAJILI TAASISI/KAMPUNI YAKO KWENYE MFUMO WA USAJILI NA USHUGHULIKIAJI WA MALALAMIKO (**RCMIS**) WA TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI (**PDPC**)

**1** INGIA KWENYE **TOVUTI** YA PDPC
Bonyeza ***www. pdpc.go.tz*** ili kuingia kwenye tovuti ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

**2** BONYEZA NENO **REGISTRATION** (USAJILI)
Ukiingia kwenye tovuti utaona picha zinaslide, shuka chini kidogo, baada ya picha hizo na bonyeza kitufe kilichoandikwa Registration.

**3** FUNGUA **AKAUNTI** YA TAASISI/KAMPUNI YAKO
Bonyeza tena kitufe kilichoandikwa Registration ili uweze kufungua akaunti ya taasisi/kampuni yako kwenye mfumo wa RCIMIS.

**4** JAZA **TAARIFA** ZA TAASISI/KAMPUNI YAKO
Jaza baadhi ya Taarifa za Taasisi/kampuni yako kama jina na barua pepe (email) ili kufanikisha zoezi la kufungua akaunti.

**5** BONYEZA NENO **CREATE ACCOUNT**
Bonyeza kitufe kilichoandikwa create account ili ukamilishe zeozi la kufungua akaunti ya Taasisi/kampuni yako.

**6** **ACTIVATE** AKAUNTI YA TAASISI/KAMPUNI YAKO
Ingia kwenye barua pepe uliyoijaza wakati wa kufungua akaunti na ubonyeze link uliyotimiwa ili kuactivate akaunti yako.
**NB:** Kwasababu za kiusalama link inakua active kwa dakikia 20 pekee

**7** **LOG IN** (INGIA) KWENYE AKAUNTI YA TAASISI/KAMPUNI YAKO
Ingia kwenye akaunti ya Taasisi/kampuni yako kupitia barua pepe na Nywila (Password) uliyojaza wakati wa kufungua akaunti na kisha bonyeza neno ***COMPLETE APPLICATION***

**8** JAZA TAARIFA ZA **AFISA ULINZI WA TAARIFA** (DPO)
Jaza Taarifa Binafsi za DPO na ambatanisha barua ya Utambulisho iliyosainiwa na Mkuu wa Taasisi/kampuni wako na kugongwa muhuri.

**9** JAZA **TAARIFA ZA TAASISI/KAMPUNI** YAKO
Jaza Taarifa za Taasisi yako na ambatanisha Vielelezo vinavyohitajika ikiwemo ***Brela Certificate, TIN Certificate, Audited Financial Year Report.***
**NB:** Kwa Taasisi za Serikali utaambatanisha ***TIN Certificate*** tu

**10** BONYEZA NENO **SUBMIT**
Bonyeza kitufe kilichoandikwa neno Submit ili kutuma maombi yako kwenye Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

**11** **HAKIKI** TAARIFA ULIZOJAZA
Baada ya kubonyeza kitufe cha Submit, utapata nafasi ya kuhakiki Taarifa zako ulizozijaza kwenye mfumo kama ziko sawa au unahitaji kuziboresha.

**12** **THIBITISHA/REKEBISHA** TAARIFA ULIZOJAZA
Bonyeza kitufe kilichoandikwa **Yes Submit!** kuthibitisha Taarifa ulizojaza au bonyeza kitufe kilochoandikwa **No Edit!** ili kuboresha Taarifa ulizojaza.

**13** PAKUA **INVOICE**
Pakua Ankara (Invoice) yako kwa kubonyeza alama ya kijumba iliyopo sehemu ya Payment.

**14** FANYA MALIPO KUPITIA **CONTROL NUMBER**
Fanya malipo kwa control number iliyoainishwa kwenye Ankara (Invoice) yako.

Kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (**NGO's)** kwenye **hatua ya 9** wataambatanisha ***NGO Certificate*** na ***TIN Certificate*** tu.


PDPC TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

## KIDOKEZO CHA ULINZI WA TAARIFA

Taasisi au kampuni inayotoa huduma kwa jamii, hakikisha unazilinda Taarifa Binafsi za watu unaowapa huduma. Ni kosa kisheria kuzitoa bila ridhaa ya muhusika wa Taarifa hizo.












@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

# MAKALA MAALUMU

## Chimbuko la Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPA)




zinazoweza kufanya mtu akatambulika, mfano Jina lake, jinsia yake, dini yake, kabila lake, namba yake ya simu, barua pepe yake, makazi yake, picha yake, kundi lake la damu (DNA), namba yake ya kitambulisho, leseni ya udereva, pasi ya kusafiria, NIDA, n.k.

Hivyo basi Taarifa yoyote ambayo unaona inaweza kukutambulisha popote pale hiyo ni Taarifa yako Binafsi na unapaswa kuilinda kama mboni ya jicho lako

Machache yameandikwa kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania, Sura ya 44 ya Sheria za Nchi (PDPA), bila shaka hayajaandikwa si kwasababu hayapo la hasha bali ni kutokana na ugeni au upya wa Sheria hii.

Makala hii imeandaliwa kwa lengo la kukupa elimu ya kina kuhusu Sheria hiyo na itaweka bayana kwanini Sheria hii ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa na jamii kwa ujumla ambapo itaangazia faida na umuhimu wa Sheria yenyewe pamoja na chimbuko lake.

Katika kuyaangazia hayo kwanza nianze kwa kukujengea uelewa kuhusu maana ya Taarifa Binafsi ambapo baadhi ya watu wanadhani Taarifa Binafsi ni siri zao au ni zile Taarifa ambazo hazifai kumshirikisha mtu yeyote yule. La hasha! Taarifa Binafsi ni zile Taarifa zinazo mtambulisha mtu au ....

jicho lako kwakua ikitumika vibaya inaweza kukuletea madhara mbalimbali ikiwemo wizi na kuharibika kwa staha au hadhi/heshima au utu wako (Reputation, Status or Dignity).

**ULINZI WA TAARIFA BINAFSI NI NINI?**

Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ni hatua zinazolenga kuzuia matumizi mabaya ya Taarifa Binafsi ili kulinda faragha ya mhusika wa Taarifa. Hatua hizo ni za kimkakati na ......

za kiutaratibu zinazochukuliwa wakati wa Ukusanyaji na/au Uchakataji wa Taarifa. Pengine unajiuliza kwa nini ulinde Taarifa zako Binafsi. Ni hivi, zipo sababu nyingi za msingi za wewe kufanya hivyo ila kwa uchache unapaswa kulinda Taarifa zako Binafsi ili:-

* Kuzuia Matumizi Mabaya ya Taarifa zako.
* kujilinda dhidi ya uhalifu wa mtandao unaoweza kusababisha madhara kwa mhusika kiuchumi, kijamii/kisiasa na kiusalama.
* Kulinda staha, heshima na utu wako;
* Kulinda amani ya moyo (Peace of mind). na
* Kuimarisha Uaminifu na Uadilifu (Trust and Integrity).



**CHIMBUKO LA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**

Haki ya Faragha inayotokana na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu ni miongoni mwa sababu za msingi zilizopelekea kuanzishwa kwa Kanuni za Jumla za Ulinzi wa Taarifa Binafsi za Umoja wa Ulaya inayotambulika kama "General Data Protection Regulations (GDPR)" ambayo ni mfumo wa kisheria wa ulinzi wa taarifa binafsi mkubwa zaidi Duniani kwa kuwa unahusisha wananchi wote wa Umoja wa Ulaya bila kujali walipo. Aidha, sababu nyingine kubwa ya umuhimu wa mfumo

kujali walipo. Aidha, sababu nyingine kubwa ya umuhimu wa mfumo wa kisheria wa ulinzi wa taarifa binafsi ni uimarishaji wa uchumi wa kidijitali.

Naam Wapwani wanasema Mcheza kwao hutunzwa na sasa tuangazie Chimbuko la Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPA) ambayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 2022 na kuanza kutekelezwa rasmi Mwaka 2023.

Chimbuko la kutunga Sheria hii ilikuwa ni kutokuwepo kwa Sheria mahsusi na Chombo cha kusimamia wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi kwa kuainisha misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi; uhitaji wa kuifanya anga ya mtandao kuwa salama kwa kuoanisha na miongozo ya Kikanda na Kimataifa;

kutekeleza maelekezo ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016; kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM (Chama tawala) ya mwaka 2020;

na umuhimu wa kuimarisha uchumi wa kidijitali pamoja na kuongeza uwekezaji kwenye Sekta ya TEHAMA nchini.

Kabla ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 ya Sheria za Nchi, Tanzania tulikuwa na Sheria kadhaa zilizoshughulikia Ulinzi wa Taarifa na faragha za watu, ambapo baadhi ya Sheria hizo ni:

**Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai - 1985:**
Sheria hii inatafsiri Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ambapo kama mtu akikiuka Haki ya Faragha, inaeleza hatua za kufata katika kushughulikia Shauri hilo.

**Sheria ya Kuzuia Ugaidi 2002:**
Sheria hii inaruhusu Taarifa Binafsi za Shahidi kutokuwekwa Hadharani yaani kufichwa ili kulinda haki yake ya Faragha na Usalama.

**Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha - 2006:**
Sheria hii inazuia wafanyakazi wa Benki kutoa Taarifa Binafsi za Wateja wao kwa Mtu au Taasisi Yoyote.

**Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta - 2010 (EPOCA):**
Sheria hii inasimamia mawasiliano ya kielektroniki, mawasiliano ya simu na posta nchini Tanzania ambapo kupitia kifungu cha 98 cha Sheria hii wafanyakazi wa Ofisi za Mawasiliano ya Simu, Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta hawaruhusiwi kutoa Taarifa binafsi za Mteja kwa Mtu au Taasisi yoyote.

**Sheria ya Makosa ya Mtandao - 2015:** Sheria hii inaweka makosa yanayohusiana na ukiukaji wa faragha dhidi ya au kutumia mfumo wa kompyuta au Mtandao nchini ambapo kupitia kifungu cha 48 cha Sheria hii Mtu yoyote haruhusiwi kuweka (publishing) Taarifa Binafsi za Mtu Mtandaoni bila Ridhaa ya muhusika wa taarifa.

**FAIDA ZA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**

Kuna faida nyingi za Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iwe kiuchumi, kisiasa au kijamii. Hapa tutaangazia faida hizi kwa Mtanzania mmoja mmoja bila kujali umri, cheo/nafasi wala jinsia na kwa Taifa kwa ujumla: -

1. **Kuifanya anga ya mtandao ya Tanzania kuwa salama kwa kuzingatia matakwa ya Mikataba na Miongozo ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi; Mikataba na Miongozo ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi.**

2. **Kuongezeka kwa matumizi sahihi ya Taarifa Binafsi nchini.**

3. **Kuongezeka kwa amani na usalama nchini.**

4. **Kuongezeka kwa watumiaji wa huduma za mtandaoni kwa uhakika wa taarifa zao binafsi kuwa salama.**

5. **Kuongezeka kwa wawekezaji wa masuala ya teknolojia nchini na kuwapatia watanzania sifa na fursa ya kuwekeza nje ya nchi hususan kupitia mifumo ya TEHAMA.**

Naomba nitamatishe Makala hii kwa kukujuza kwamba Ulinzi wa Taarifa Binafsi unaanza na wewe mwenyewe hivyo linda Taarifa zako kwa kuhakikisha unazitoa pale zinapohitajika tu kulingana na huduma unayohitaji yaani kama unahitaji huduma ya kupewa cheti/vyeti basi toa Taarifa ambazo zinahusiana na wewe kupata hivyo vyeti , sio unahitaji Leseni ya Biashara wakulazimishe kutoa Taarifa ya Idadi ya Watoto ulionao hiyo sio sawa.

TUME YA
ULINZI WA
TAARIFA BINAFSI



## WASILIANA NASI


Huduma kwa wateja:
0718462536, | 0736110505, | 0744057652
0695507751, | 0753459155, | 0615779070

*Baruapepe: helpdesk@pdpc.go.tz*


Au tufuatilie kwenye mitandao ya kijamii;

@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

Channels

Pia unaweza kujiunga na Chaneli yetu ya WhatsApp kwa jina la Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)